# Maswali na Majibu

Powered By INJILI MILELE

**Januari 24, 2025**

Mch. Almodad Amos Yaragwiller

Ep. 003

## MADA: SABATO YA JUMA LA UUMBAJI

# Sabato ni nini?

### Utangulizi

Kuna angalau aina 49 za Sabato katika Biblia, na hii inafanya wengi wasiochunguza mambo wadhani Sabato ni sabato tu. Kuacha hizo aina nyingine za Sabato, hapa tutazungumzia aina moja tu ya Sabato, Sabato ya Juma la Uumbaji. Sabato hii, ni siku ya saba ya juma ambayo Mungu aliitenga, kwanza, kuwa takatifu kwa makusudi ya kuadhimisha kazi kubwa ya uumbaji iliyofanyika kwa siku sita, na pili kuwa ishara kati ya Mungu na watu wake.

### Sabato ni Siku

Ni muhimu sana kuelewa kuwa Sabato ni siku. Huu ni muda maalum sana tangu Ijumaa jua linapozama mpaka jua linapozama tena Jumamosi. Na kwa sababu Mungu aliitenga, kwa maana ya kuibariki na kuitakasa, haiwezi kuwa siku nyingine yoyote ile. Ni sehemu ya amri kwamba siku hii inapaswa kuwa siku ya Saba ya juma, yaani Jumamosi, na si vinginevyo. Biblia inasema:

> **Mwanzo 2:2,3 SUV**
> 2 Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. 3 Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.

> **Kutoka 20:9,10 SUV**
> Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. 9 Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; 10 lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako.

Upekee wa siku hii tofauti na siku nyingine ni kwamba, siku hii imebarikiwa na imetakaswa na Mungu mwenyewe. Waweza kuchagua siku unayoitaka wewe na kuiita Sabato, lakini ukumbuke haikubarikiwa na haikutakaswa na Mungu.

## Sabato ni Ishara

Sabato ni ishara kwamba Mungu ndiye aliyeiumba dunia hii, lakini pia Sabato ni ishara kwamba sisi tumeokolewa. Hatuitunzi Sabato ili tuokolewe, kunyume chake tunaitunza Sabato kama matokeo ya kuokolewa kwa neema ya Bwana.

> **Ezekieli 20:12, 20 SUV**
> zitakaseni sabato zangu; zitakuwa ishara kati ya mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu.

## Sabato ni Amri

Tunapoitunza Sabato tunakiri kwa vitendo kwamba hatuwezi kujisafisha dhambi zetu wenyewe.

> **Kumbukumbu la Torati 5:12 SUV**
> Ishike siku ya Sabato uitakase, kama BWANA, Mungu wako, alivyokuamuru.

## Hitimisho

Sabato ni siku takatifu iliyowekwa na Mungu kama kumbukumbu ya uumbaji na ishara ya uhusiano wake na watu wake. Kwa kuitunza Sabato, tunakiri ukuu wa Mungu kama Muumbaji na Mwokozi wetu.

Asante kwa kusoma na kufuatilia makala hii, unaruhusiwa kuisambaza kwa wengine pia. Huduma hii inafanywa na Injili Milele, na hapa chini kuna Button ambayo unaweza kuibofya ili kutazama na kusikiliza Video nyingine nyingi zinazotengenezezwa na Injili Milele. Ikiwa unamaswali au mapendekezo kuhusu mada ambazo wakati ujao tuziandikie makala za namna hii tafadhali usisite kuwasilisha maswali na maoni yako kupitia namba za simu au barua pepe kama ifuatavyo:

Simu/WhatsApp: +255718 834 621
Barua Pepe: modaofhope4u@gmail.com
Tovuti: imeandikwa.adventistafrica.org

Bofya Hapa Kutazama Video ya Somo Hili

YouTube Injili Milele